



# MAJARIBIO YA MTHANI GREDI YA 3 MUHULA WA I-2019 KISWAHILI

Jina \_\_\_\_\_

Shule \_\_\_\_\_

Tarehe \_\_\_\_\_

## Imla

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_
4. \_\_\_\_\_
5. \_\_\_\_\_

## Andika sentensi hizi kwa umoja

6. Wakulima wale watapanda mahindi.  
\_\_\_\_\_
7. Majani haya ni ya miti ile.  
\_\_\_\_\_
8. Misumari hii ni yangu.  
\_\_\_\_\_
9. Ng'ombe hawa ni wanene.  
\_\_\_\_\_
10. Haya ni mavazi marefu.  
\_\_\_\_\_

## Andika idadi hii kwa maneno

11. 211 \_\_\_\_\_
12. 370 \_\_\_\_\_
13. 125 \_\_\_\_\_
14. 459 \_\_\_\_\_
15. 230 \_\_\_\_\_

## Jaza mapengo

16. M \_\_\_\_ w \_\_\_\_ ng \_\_\_\_
17. F \_\_\_\_ br \_\_\_\_ ar \_\_\_\_
18. B \_\_\_\_ nd \_\_\_\_ r \_\_\_\_
19. T \_\_\_\_ if \_\_\_\_

20. K \_\_\_\_ ch \_\_\_\_ nj \_\_\_\_ o

**Ambatanisha neno na maana sahihi**

21. Hali ya kutokuwepo Imara na vita.
  22. Wakati wa jua kali Sherehe bila mvua.
  23. Shughuli za kufurahia Amani jambo.
  24. Hali ya ukakamavu. Kiangazi.
- Kanusha sentensi hizi**
25. Ninapika wali wa mgeni.  
\_\_\_\_\_
  26. Viatu hivi vinaoshwa.  
\_\_\_\_\_
  27. Nilimpigia simu.  
\_\_\_\_\_
  28. Tulioga asubuhi.  
\_\_\_\_\_

**Tumia maneno yaliyo kwenye jedwali kujaza pengo**

**babu, likizo, takataka, mama**

29. Shimoni ni mahali pa kutupa  
\_\_\_\_\_
30. Wakati wa mapumziko ni  
\_\_\_\_\_
31. Baba yake baba ni \_\_\_\_\_
32. Mzazi wa kike \_\_\_\_\_

**Kamilisha sentensi ukitumia**

**haraka na polepole**

33. Mwanafunzi mzuri huandika \_\_\_\_\_

34. Gari kuukuu huendeshwa \_\_\_\_\_

35. Ukichelewa kuamka unafaa kwenda shuleni kwa mwendo wa \_\_\_\_\_

**Tegua vitendawili vifuatavyo**


36. Mchana yuko usiku simuoni \_\_\_\_\_

37. Mzee Kobe akilia watu hufurahi \_\_\_\_\_

38. Changaa chapendeza lakini hakifikiwi \_\_\_\_\_


**Andika majina ya picha**

39.



\_\_\_\_\_

40.



\_\_\_\_\_

41.



\_\_\_\_\_

42.



\_\_\_\_\_

**Jaza mapengo ukitumia**

**maneno yafuatayo**

**chini, juu, ndani**

43. Vitabu vya mwalimu viko \_\_\_\_\_ ya meza.

44. Nimeweka maji \_\_\_\_\_ ya chupa.

45. Mtoto mtundu amejificha \_\_\_\_\_ ya kitanda.

46. Maembe yako \_\_\_\_\_ ya mti.

**Soma ufahamu kisha ujibu**

**maswali**

Shughuli zilikuwa nyingi jijini

Sokomoko. Mama Bidii alikuja sokoni kununua nyama na kusaga mahindi kwenye mtambo.

Alipofika kwenye buchari, aliuweka mkoba wake chini. Alijiunga na wanunuzi wengine ili apimiwe nyama kwa ratili. Foleni iliposonga, aliinama kuusongesha mkoba wake lakini haukuwepo. Mwizi alikua amechukua.

47. Mama Bidii alienda sokoni kufanya nini? \_\_\_\_\_

48. Mkoba wa Mama Bidii ulienda wapi? \_\_\_\_\_

49. Nyama ilipimwa kutumia nini? \_\_\_\_\_

50. Mama Bidii alienda sokoni jiji lipi? \_\_\_\_\_